OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

Kumb.Na.LSS/J.I/F...../202....

KWA MZAZI/MLEZI WA:

.....
.....
.....

YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUMO</u>

1. UTANGULIZI

Ninafuraha kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 202.....

Shule ya Sekondari **LUMO** ipo Halmashauri ya **Manispaa ya Temeke** Tarafa ya Mbagala **Kata ya Yombo Vituka** Mtaa wa **Magogoni**

Shule inafikika kwa urahisi kwa usafiri wa mabasi ya umma kutoka katikati ya jiji na pembezoni mwa jiji la Dar es salaam

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ...../...../20….. unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe.....na mwisho wa kuripoti ni tarehe.....ndani ya siku kumi na nne (14).

EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(A). SARE ZA SHULE

Ushonaji wa sare za shule uzingatiwe:

- zingatie vipimo na muonekano wa mchoro wa mshono ulioonyeshwa kwenye ukurasa wa tatu (3) usizidishe wala usipunguze

(i) <u>WASICHANA</u>

SKETI YA HIJABU: Ifike kwenye kifundo cha miguu

NUSU KANZU: Ifunike makalio

- Ichanwe pembeni sm 4 kutoka chini

- Isiwe modo
- Nyeupe na juba jeupe refu ifunike kifua

SKETI YA KAWAIDA: Iwe sm 15 kuanzia chini ya goti

- Iwe na belt sm 4
- Pindo sm 2

VIATU: Vyeusi vya ngozi vyenye kamba
Visiwe na kisigino kirefu

SOKSI: Nyeupe ndefu zisizo na urembo

SHATI: Nyeupe mikono mifupi

(ii). WAVULANA:

SURUALI: Urefu ifike kwenye kisigino

- Iwe na marinda mawili mbele
- Iwe na pindo chini la nje
- Upana wa suruali chini iwe sm 15 hadi sm 16
- Iwe na mifuko miwili mbele na mmoja nyumba
- Iwe na ruksi sita za kuwekea mikanda

SHATI: Nyeupe mikono mifupi

VESITI: Nyeupe isiwe ya rangi

MKANDA: Mweusi wa ngozi wenye kifungio cha kawaida

SOKSI: Nyeusi ndefu zisizo na urembo

VIATU: Vyeusi vya ngozi vyenye kamba visiwe na visigino virefu

LUMO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

MSHONO WA SARE ZA SHULE

SKETI – WASICHANA





SURUALI – WAVULANA





(B). VIFAA VYA KUJIFUNZIA:-

1. Madaftari makubwa kumi (10) (Counter Books Quire 3)
2. Kalamu na mkebe (Mathematical set)
3. Rula ndefu ya sm 30
4. Begi jeusi la kubeba mgongoni kubwa la kutosha kutunzia madaftari
5. Madaftari madogo kwa ajili ya mazoezi kulingana na idadi ya masomo wanayosoma.

(C). USAFI

1. Usafi wa mwili na mavazi ni muhimu uzingatiwe kila siku
2. Nywele fupi na nadhifu zisiwe na mtindo wa aina yoyote
3. Njiti ya kiberiti ionekane na zichanwe vizuri
4. Wasichana hawaruhusiwi kusuka

(III). KUCHA:

1. Ziwe fupi zisipakwe rangi wala hina

(IV). NGOZI:

1. Ngozi iwe safi, isipakwe vichubua ngozi
2. Ibaki kwenye uasili wake

(V). MAZINGIRA:

1. Ni wajibu wa mwanafunzi kusafisha na kutunza mazingira ndani na nje ya darasa
2. Ratiba ya usafi izingatiwe
3. Matumizi sahihi ya vitunza taka
4. Ni marufuku kwa wanafunzi kutupa taka ovyo

LUMO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

(D). MZAZI/MLEZI:

1. Ahakikishe mwanafunzi anapata chakula muda wote awapo shuleni
2. Mwanafunzi anayetumia usafiri apatiwe nauli ya kwenda na kurudi shuleni
3. Ahakikishe anamtimizia mwanafunzi mahitaji yote muhimu
4. Ahakikishe mwanafunzi anafika shuleni siku zote za masomo. Kama kuna dharura ahakikishe taarifa zinafika shuleni kwa wakati
5. Ahakikishe anakuwa na mawasiliano ya karibu na mwalimu wake wa darasa

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Nilazima kuheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
3. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wanafunzi wawapo shuleni
5. Kutunza usafi wa mwili wako na mazingira ya shule
6. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa na ivaliwe kwa heshima kama ilivyoelekezwa
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
8. Si ruhusa kuwa na simu katika mazingira ya shule
9. Si ruhusa kusuka nywele au kunyoa mitindo au kufuga ndevu kwa wavulana
10. Si ruhusa kuweka dawa kwenye nywele aidha kupaka rangi/hina kwenye kucha za vidole/mikononi/mwilini.
11. Kushiriki kwa makini kwenye masomo kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

LUMO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

UTAWALA

4. MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

a) WIZI
b) UASHERATI/UBAKAJI/USHOGA
c) ULEVI WA AINA YOYOTE
d) UVUTAJI WA SIGARA/BANGI/UTUMIAJI WA DAWA ZA KULEVYA
e) MAKOSA YA JINAI
f) KUPIGANA AU KUPIGA
g) KUHARIBU MALI YA MTU/UMMA/FEDHA YA SERIKALI KWA MAKUSUDI
h) KUDHARAU BENDERA YA TAIFA/VIONGOZI WA SERIKALI
i) KUOA NA KUOLEWA
j) KUPATA MIMBA/KUMPA MWANAMKE MIMBA
k) KUSHIRIKI MATENDO YA UHALIFU, SIASA NA MATENDO YOYOTE YALE YANAYOVUNJA SHERIA ZA NCHI.
l) KUTEMBELEA MAJUMBA YA STAREHE NA NYUMBA ZA KULALA WAGENI
m) KUTOA MIMBA/KUSHIRIKI KATIKA KUTOA MIMBA
n) KUTOHUDHURIA VIPINDI VYA DARASANI KWA ZAIDI YA SIKU 90 BILA TAARIFA/UTORO
o) KUTOA LUGHA CHAFU KWA WANAFUNZI WENZAKE,WALIMU/WALEZI NA JAMII KWA UJUMLA
p) KUFUGA NDEVU AU NYWELE NDEFU
q) KUGOMA, KUCHOCHEA AU KUONGOZA AU KUVURUGA AMANI NAN USALAMA WA SHULE AU WATU
r) KUFANYA JARIBIO LOLOTE LA KUJIUA, AU KUTISHIA KUJIUA KAMA KUNYWA SUMU N.K
s) KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI
t) KUTOKA NJE YA SHULE AU KUKUTWA NJE YA ENEO LA SHULE WAKATI WA MASOMO BILA KIBALI
u) KUMILIKI, KUKUTWA AU KUTUMIA SIMU YA MKONONI/LINE YA SIMU/CHARGER KATIKA MAZINGIRA YA SHULE

---

5. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA. MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA SHULE. NA ADHABU NYINGINE KUTOKANA NA KOSA

a) Kutohudhuria shuleni bila sababu
b) Kutoroka shule au kutoroka vipindi bila ruhusa
c) Kutovaa sare za shule kwa usahihi
d) Kuandika maneno ukutani, kwenye dawati, mbao za shule au mtaani (atafidia uharibifu)
e) Kukanyaga au kukaa juu ya dawati
f) Kukaa nje wakati vupindi vinaendelea
g) Kutoandika nukuu za masomo (Notes)
h) Kutofanya mitihani yoyote inayotolewa shuleni
i) Kuchelewa, kupiga kelele darasani na kuondoa utulivu katika eneo la shule kufanya mijadala isiyo na manufaa kitaaluma na kinidhamu
j) Kuwa na vitu visivyo na mchango kitaaluma kama CD, Flash, Picha, Mavazi, Cheni,Hereni, na Perfume

Mwanafunzi atanyanganywa na hatarejeshewa.

EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

6. MIPAKA YA SHULE

a) Mipaka ya shule ipo wazi na mwanafunzi atakapofika ataonyeshwa

b) Hairuhusiwi kutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali

c) Saa za kutoka nje ya mipaka hiyo zimeoneshwa kwenye ratiba ya shule

(D). Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-

i. Chumba maaalumu kwa walimu (Staff Room)

ii. Ofisi za shule (School Offices)

iii. Maabara

iv. Jikoni

(E). Ni marufuku mwanafunzi kuonekana sehemu zifuatazo:-

i. Vilabu vya pombe (Bar, Night Clubs, Vigodoro)

ii. Majumba ya starehe

iii. Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses and Lodge)

MUHIMU

Mwanafunzi hatapokelewa shuleni kama hakukamilisha mahitaji na kujaza kwa ukamilifu Fomu namba **1, 2, 3** na **4.**

LUMO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS A RIGHT OF LIFE

.....

FRIDA I. KYANDO

MKUU WA SHULE

FOMU NO. 1

SHULE YA SEKONDARI LUMO

HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijanzwe na Mwanafunzi)

1. (i) Jina la mwanafunzi.....

(**NB.** Jina hili ni **LAZIMA** liwe lile la kwenye **TSM 9** libaki hivi kwa kipindi chote utakachokuwa katika shule hii).

Shule atokayo.....

(ii) Tarehe ya kuzaliwa.....Wilaya.....Mkoa.....

(iii) Dini.....Dhehebu.....

(iv) Shule ulizosoma kabla ya kuja Lumo Sekondari

JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI	SHULE YA MSINGI/SEKONDARI	KIPINDI ULICHOSOMA
1.		
2.		
3.		
4.		

Saini ya Mwanafunzi.....

2. **AFYA**

(i) Taja magonjwa yoyote makubwa uliowahi kuugua mfano: TB, Polio, Kifafa nk.

.....

(ii) Taja matatizo ya afya yako.....

3. **JINA LA MZAZI**

(i) Mama .....Hai/amefariki lini.....?

(ii) Baba ..... Hai/amefariki lini.....?

KAZI YA

(iii) Baba .....Dini.....Dhehebu.....

(iv) Mama ..... Dini.....Dhehebu.....

(v) Anuani ya Mzazi kwa sasa: S.L.P.....wilaya.....mkoa.....

IJANZWE NA MWENYEKITI WA MTAA

4. JINA LA MTAA.....

JINA LA MWENYEKITI.....

. UTHIBITISHO – NI MKAZI/SIO MKAZI (Kata isiyo sahihi)

NAMBA YA SIMU.....

SAHIHI ..... **MHURI……**

LUMO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

FOMU NO. 2

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TECHNOLOGIA NA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI LUMO

FOMU YA KUANDIKISHWA

IJANZWE NA MWANAFUNZI:

Jina kamili la mwanafunzi.....

1. Taifa.....
2. Uraia.....
3. Dini.....
4. Tarehe ya kuzaliwa.....
5. Shule ya msingi.....
6. Mwaka aliomaliza.....
7. Cheti cha kuzaliwa.....

Sahihi ya mwanafunzi.....

PICHA YA MWANAFUNZI

MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la mzazi/mlezi.....
2. Anuani kamili ya mzazi/mlezi.....
3. Mkoa/Wilaya/Kata anayoishi.....
4. Mtaa.....
5. Nambari ya nyumba.....
6. Nambari ya simu ya nyumbani (**landline**).....
   Ya mkononi.....

Sahihi ya mzazi/mlezi.....

PICHA YA MZAZI/MLEZI

EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/MLEZI

1. Jina la mwajiri na Idara.....
2. Anwani yake.....
3. Nambari ya simu.....
4. Kazi ya mzazi/mlezi (meneja,karani,daktari,mfanyabiashara n.k).....

SOMO LA DINI

Mimi.....ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi..... Kidato cha.....ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria soma la Dini ya .....Dhehebu la .....Siku ya Jumatano akiwa shuleni Lumo.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.....

FOMU NO. 3

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI LUMO
DAR ES SALAAM

KWA MWANAFUNZI:

Mimi..... (Jina kamili)

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha.....mwaka.....katika shule ya Sekondari Lumo. Naahidi kwamba:-

1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2. Nitatia bidii katika masomo,kazi na shughuli zote za shule ili kufikia malengo ya shule kwa ufanisi
3. Kitashiriki kikamilifu katika shughuli za kutunza mazingira ya shule na uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyobora bila kuitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza mali ghafi (Raw material) yakuzalishia mali
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Sekondari Lumo.

MUNGU NISAIDIE

Sahihi ya Mwanafunzi.....

KWA MZAZI/MLEZI

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi).....

Mzazi/Mlezi wa.....

Naahidi kwamba:-

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (Maoni,adhabu) katika kumlea mwanangu
3. Nitamlinda mwanangu na kumsimamia kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.....

LUMO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

FOMU NO. 4

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

STATION:.....

DATE:.....

PART A:

TO:

Medical Officer

.....

.....

Miss/Mr.....

Please examine the above named as to his/her fitness for admission as a student in the following common diseases/ problems:-

Put a tick (√) for positive and a cross (X) for negative against in a box provided.

Pregnancy	
Asthma	
Sight	
Diabetes	
Worms (stool)	
Epilepsy	
TB (Tuberculosis)	
Sickle cell	
Heart disease	
Yellow fever	
U. T. I	
Hearing	

LUMO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS A LIGHT OF LIFE

PART B. MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named and consider that she/he is physically FIT/ UNFIT for admission as above

Date..... **Signature**.....

Station..... **Designation**.....